

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU



Zanzibar

10 Disemba, 2024

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amewataka Mawaziri kuwatumia ipasavyo Makatibu Wakuu na wataalamu wataowakuta katika Wizara zao ili kuongeza ufanisi ndani ya Serikali katika kuwashudumia wananchi.

Rais Dkt. Samia ameyasema hayo leo Ikulu ndogo ya Tunguu wakati akiwaapisha Viongozi mbalimbali wakiwemo Mawaziri, Naibu Mawaziri, Naibu Makatibu Wakuu na Mabalozi wateule.

Aidha, Rais Dkt. Samia amesema katika kutekeleza mkakati wa taifa wa uchumi wa kidigitali ambao unachochewa na kasi ya ukuaji wa sekta ya mawasiliano na teknolojia ndani ya nchi na dunia nzima, ni vyema sasa kutenganisha majukumu hayo na yale ya sekta ya habari ili msisitizo wa kimkakati utekelezwe kwa ufanisi zaidi.

Kwa upande mwingine, Rais Dkt. Samia amemuagiza Waziri wa Mifugo na Uvubi, Mhe. Ashatu Kijaji kuchochea ufanisi na uimarishaji wa uchumi wa buluu pamoja na kuambatana na wataalamu katika kuwasikiliza na kutatua kero za wakulima na wafugaji.

Rais Dkt. Samia pia amemtaka Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano wa Mazingira) Mhe. Hamad Yussuf Masauni kushughulikia ipasavyo masuala ya Muungano na kumtaka kushiriki kikamilifu katika majukwaa mbalimbali ili kunapaza sauti kimataifa kuhusu masuala ya mazingira.

Vile vile, Rais Dkt. Samia amewataka Mabalozi wapya kwenda kuiwakilisha vyema Tanzania hasa katika maeneo ambayo kama taifa tuna maslahi nayo hasa zile nchi tulizoshirikiana nazo katika ukombozi wa Bara letu la Afrika.

Sharifa B. Nyanga
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu



Ikulu Mawasiliano / ikulu_mawasiliano /
ikulu_Tanzania / ikulu_Tanzania /
ikulumawasiliano / Ikulu Tanzania / Ikulu Tanzania



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU**

